TANGAZO LA SERIKALI NA. 354 la tarehe 26/4/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

AMRI

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI NA USAFI WA MAZINGIRA HANDENI (HTMWSSA) MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA HANDENI TRUNK MAIN, 2019

Jina

1. Amri hili litajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni ("HTM WSSA"), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira, 2019.

Tarehe ya Kuanza

2. Amri hii litaanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Mei, 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za HTM WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4.-Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 Julai, 2019 au kabla, HTM WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hili.

(b) HTM WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

(c) HTM WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

(d) Ifikapo tarehe 30 Juni 2019 au kabla, HTM WSSA itahakikisha mtambo wa kutibu maji unakuwa na umeme.

(e) Ifikapo tarehe 30 Juni 2019 au kabla, HTM WSSA itahakikisha kuwa matanki yote ya kuhifadhia maji yanawekewa valvu ili kuzia maji yanapojaa kumwagika.

(f) HTM WSSA ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA.

(g) HTM WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne.

(h) HTM WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA.

(2) Taarifa zilizowasilishwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1)(h) zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa HTM WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

(3) EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na HTM WSSA katika siku zijazo.

Kufutwa Amri Na. 13-002 la tarehe 1 Machi 2013

5. Amri hii inafuta matumizi ya Amri Na. 13-002 ya tarehe 1 Machi, 2013 katika maeneo yanayohudumiwa na HTM WSSA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

	Bei za Sasa	**Bei Zilizoidhinishwa**		
Kundi la Wateja	**2017/18**	**2018/19**	**2019/20**	**2020/21**
Majumbani	1,360	2,500	3,600	4,000
Taasisi	1,490	2,800	4,000	4,400
Biashara	1,610	3,000	4,300	4,700
Viwanda/ Umwagiliaji	1,880	3,500	5,000	5,500
Maji ya jumla	910	1,700	2,400	2,700
Unyweshaji mifugo	910	1,700	2,400	2,700
Magati	1,360	2,500	3,600	4,000
Wastani Linganisho	**1,338**	**2,473**	**3,549**	**3,935**

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	**Tozo ya Sasa**	**Tozo Zilizoidhinishwa**		
	2017/18	**2018/19**	**2019/20**	**2020/21**
Majumbani	1,500	Tozo hairuhusiwi		
Taasisi	1,500			
Biashara	1,500			
Viwanda/ Umwagiliaji	1,500			
Magati	1,500			
Maji ya jumla	1,500			
Unyweshaji Mifugo	1,500			

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Majisafi za mwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda/ Umwagiliaji				
Magati				
Maji ya jumla				
Unyweshaji Mifugo				

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	11,000.00	20,000	20,000	20,000
Taasisi	14,000.00	20,000	20,000	20,000
Biashara	15,000.00	20,000	20,000	20,000
Viwanda/ Umwagiliaji	20,000.00	20,000	20,000	20,000
Magati	11,000.00	20,000	20,000	20,000
Maji ya jumla	20,000.00	20,000	20,000	20,000
Unyweshaji Mifugo	20,000.00	20,000	20,000	20,000

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

Maelezo ya uwekezaji mpya, mabadilisho ya miundombinu na ukarabati	2018/19	2019/20	2020/21
	Kiasi (Shilingi kwa maelfu)		
Kununua na kubadilisha air na sluice valvu		105,000	480,250
Kununua na kuweka dira zilizoharibika 1578 mwaka wa pili na 722 mwaka wa tatu. Pia kununua dira za wateja wapya 364 mwaka wa 2 na 314 mwaka wa 3.		186,777	104,622
Kununua pikipiki 2 mwaka wa pili na 5 mwaka wa tatu.		5,250	15,250
Purchase a car			100,000
Kununua computa mpakato 2		3,000	
Kununua mashine ya kutolea nakala moja.			5,775
Kununua meza 6 za ofisi		5,250	

Maelezo ya uwekezaji mpya, mabadilisho ya miundombinu na ukarabati	2018/19	2019/20	2020/21
	Kiasi (Shilingi kwa maelfu)		
Kununua viti 6 vya ofisi		3,780	3,780
JUMLA		309,057	709,677

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2018/19	2019/20	2020/21
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na		364	722
Kiwango cha upotevu wa maji	%	70	65	50
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato (bila madeni)	%	90	92	95

JEDWALI LA NNE
MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI MILIONI)

Gharama	2018/19	2019/20	2020/21
Uzalishaji	357.77	371.41	490.11
Umeme kwa ajili ya uzalishaji	538.94	538.94	538.94
Usambazaji	50.75	50.75	50.75
Matengenezo	270.46	282.55	389.06
Watumishi	627.20	666.57	711.81
Utawala	182.45	191.70	201.41
Matangazo	2.48	2.60	2.73
Matukio	1.23	1.32	1.41
Bodi	45.60	49.38	53.50
Fedha	3.71	3.90	4.09
Jumla ya Uendeshaji na Matengenezo	2,080.60	2,159.12	2,443.82
Uchakavu	241.85	299.08	281.05
Faida ya Uwekezaji	14.46	55.39	81.28
Jumla ya Mahitaji ya Fedha Requirement	2,336.91	2,513.58	2,806.15
Ondoa Fedha zingine zisizotokana na mauzo ya maji	342.92	359.70	377.15

Gharama	2018/19	2019/20	2020/21
Mahitaji ya fedha yanayotokana na mauzo ya maji	1,993.99	2,153.88	2,429.00

Dodoma,
11 Aprili, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY,
Mkurugenzi Mkuu